

Dar es Salaam wanachukuliaje utawala?

Maoni ya wakazi kuhusu huduma, sera na viongozi



Utangulizi

Pamoja na kupiga kura, wananchi pia wanaweza kushiriki katika michakato ya kidemokrasia kwa namna nyingine mbalimbali. Watu wanaweza kushiriki katika mikutano ya kijamii, kujadili matatizo yao na maafisa wa serikali, kupiga simu kwa waendeshaji wa vipindi vya redio au runinga na kutoa maoni yao au kuandamana kwa amani mitaani. Ushiriki wa kila siku wa wananchi wa namna hii unaonekana kuwa namna bora zaidi ya kujenga kuaminiana kati ya wananchi na viongozi wanaowatawala, na una umuhimu mkubwa katika kuimarisha uwazi, uwajibikaji na matokeo yanayotarajiwa katika utoaji huduma.

Je, wakazi wa Dar es Salaam, jiji kubwa kuliko yote nchini Tanzania, wanachukuliaje suala la ushiriki wa wananchi na utawala, na uhusiano wake na utoaji wa huduma kwa wananchi?

Ili kupata majibu ya swali hili, Uwazi iliyopo Twaweza ilifanya utafiti kwa wakazi wa Dar es Salaam katika kipindi cha Agosti na Septemba 2010. Utafiti huu ulihusisha kaya 550 katika manispaa za Ilala, Kinondoni na Temeke. Wahojiwa waliulizwa maswali kuhusu maoni yao juu ya upatikanaji wa huduma na namna wanavyokabiliana na changamoto za upatikanaji wa huduma katika maeneo yao.

Muhtasari huu unaonyesha baadhi ya matokeo muhimu ya utafiti. Unaonyesha kuwa:

- Idadi kubwa ya wahojiwa hawaridhishwi na hali ya upatikanaji wa huduma kwa wananchi, japo wachache sana wanachukua hatua kubadilisha hali hii katika maeneo yao;



Muhtasari huu umeandikwa na Dorica Andrew chini ya uangalizi wa Rose Aiko, na kuchapishwa na Uwazi iliyopo Twaweza –Hivos Tanzania.

S.L.P. 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu +255 22 266 4301. Nukushi +255 22 266 4308.
Barua pepe: uwazi@twaweza.org.
Tovuti: www.twaweza.org/go/uwazi




- Karibu nusu ya wahojiwa hawamjui Mbunge wao; na
- Idadi kubwa ya wahojiwa hawafahamu kuhusu masuala muhimu ya kisera

Mambo makuu tisa kuhusu utawala na hatua wanazochukua wananchi wa Dar es Salaam

Jambo la 1: Wahojiwa wengi wanaamini kwamba serikali haishughuliki huduma za msingi kwa umakini unaostahili

Utafiti unaonyesha kwamba wananchi hawaridhishwi na namna ambavyo huduma mbalimbali za kijamii zinatolewa. Zaidi ya asilimia 75 ya wahojiwa wamesema kwamba huduma za maji taka na mifereji ya maji machafu zinzotolewa na mamlaka za serikali haziridhishi/zinafanyika vibaya. Vilevile wengi wao wanafikiri kwamba huduma za afya na usambazaji wa maji safi na salama hazishughulikiwi ipasavyo (Kielelezo cha 1).

Kielelezo cha 1: Asilimia ya wakazi wanaoamini serikali/mamlaka zinazohusika zinashughulikia masuala mbalimbali “vibaya sana” au “kwa kiasi fulani vibaya”



Chanzo cha data: Uwazi, Public Service Delivery Survey, Dar es Salaam, 2010

Jambo la 2: Wananchi wana imani na mahakama na polisi kuliko DAWASCO na TANESCO

Zaidi ya sehemu tatu ya tano ya wahojiwa walionyesha kuwa na imani zaidi na mahakama (asilimia 65) na polisi (asilimia 62) kuwa ni taasisi zinazotoa huduma kwa manufaa ya wananchi. Karibu kiwango hicho hicho cha wahojiwa (asilimia 61) walieleza kuwa wana imani na Tume ya Taifa ya Uchaguzi.


Hata hivyo, kuhusu kampuni za ugavi wa huduma za maji na umeme kwa wananchi, wakazi wa Dar es Salaam hawaoni kama kampuni hizi zinatekeleza shughuli zao kwa manufaa ya wananchi. Ni asilimia 29 tu ya wahojiwa ndio walioonyesha kwa kiasi fulani kuwa na imani na Kampuni ya Dar es Salaam ya Maji Safi na Maji Taka (DAWASCO¹). Asilimia 43 ya wahojiwa walionyesha kuwa na imani na Kampuni ya Umeme Tanzania (TANESCO²), kikiwa ni kiwango cha juu kidogo ikilinganishwa na kile wahojiwa walichokionyesha kwa DAWASCO.

¹ Dar es Salaam Water and Sewerage Company.

² Tanzania Electric Supply Company.

Viwango mbalimbali vilivyoonyeshwa vya kuwa na imani na kampuni zinazotoa huduma vinarandana na mitazamo waliyoinyesha wahojiwa kuhusu hali ya upatikanaji wa huduma za maji salama na umeme. Kama Kielelezo cha 1 kinavyoonyesha, kuna wananchi wengi zaidi wanaofikiri kwamba huduma ya umeme inatolewa vizuri kuliko wale wanaofikiri kwamba huduma za maji safi na maji taka zinatolewa vizuri.

Kielelezo cha 2: Asilimia ya wahojiwa “wanaoiamini” au “wanaoiamini kwa kiasi fulani” mamlaka kufanya kazi kwa manufaa ya wananchi




Chanzo cha data: Uwazi, Public Service Delivery Survey, Dar es Salaam, 2010

Jambo la 3: Zaidi ya nusu ya wahojiwa wanaamini rushwa inaongezeka

Japo watu wanaonyesha kuwa na imani na polisi na mahakama za sheria kwa kiasi fulani, zaidi ya nusu ya wahojiwa (asilimia 58) wanafikiri kwamba rushwa imeongezeka nchini kuliko ilivyokuwa miaka mitano iliyopita. Karibu theluthi (asilimia 29) ya wahojiwa wamesema kuwa katika kipindi cha miezi 12 iliyopita walijikuta katika mazingira ambamo walilazimika kutoa rushwa ili wapate huduma katika kituo cha afya, mahali ambapo huduma hiyo inapaswa kutolewa bure. Zaidi ya mtu mmoja katika wahojiwa 10 (asilimia 12) pia walisema walitoa rushwa kwa polisi ili kuepuka kutozwa faini au kupata adhabu nyingine.

Kielelezo cha 3: Maoni ya wananchi kuhusu jinsi rushwa ilivyobadilika nchini katika kipindi cha miaka mitano




Chanzo cha data: Uwazi, Public Service Delivery Survey, Dar es Salaam, 2010

Jambo la 4: Viongozi wa kidini wanaaminiwa zaidi kufanya kazi kwa maslahi ya wananchi

Wananchi wana imani kubwa kwa viongozi wa kidini. Katika kujibu swali “ni kwa kiasi gani una imani kuwa viongozi wafuatao wanafanya kazi kwa maslahi ya wananchi na sio kwa manufaa yao binafsi?”, takriban asilimia 91 ya wahojiwa walisema wana imani na viongozi wa kidini “kwa kiasi kikubwa” au “kwa kiasi fulani”. Ilivutia kuona kwamba idadi kubwa ya wahojiwa (asilimia 84) walisema wana imani na Rais, wakati ambapo chini ya nusu ya wahojiwa (asilimia 44) walisema wanamwamini Mbunge wao wa kuchaguliwa. Kama nusu tu ya wahojiwa (asilimia 56) ndio walionyesha kuwa na imani na mwalimu mkuu wa shule kufanya kazi kwa manufaa ya wananchi.

Kielelezo cha 4: Asilimia ya wahojiwa ambao “wanawaamini sana” au “wanawaamini kwa kiasi fulani” viongozi kufanya kazi kwa maslahi ya wananchi badala ya manufaa yao wenyewe



Chanzo cha data: Uwazi, Public Service Delivery Survey, Dar es Salaam, 2010

Jambo la 5: Wakazi wachache wana taarifa sahihi kuhusu masuala ya sera


Watu wengi wanaamini kwamba kuongezeka kwa vyombo vya habari kumewasaidia wakazi wa Dar es Salaam kujua mambo mbalimbali kuhusu sera za kijamii, kisiasa na kiuchumi nchini. Hata hivyo, utafiti wetu umebaini kuwa ni wahojiwa wachache ndio walikuwa na ufahamu sahihi juu ya mambo yanayoelezwa katika sera (tazama Kielelezo cha 5). Kwa mfano, japokuwa Tanzania ilizundua na inatekeleza “Mkakati wa Mapinduzi ya Kijani katika Kilimo” (Kilimo Kwanza) tangu mwaka 2009, wahojiwa wapatao 8 kati ya 10 ama walikuwa kamwe hawajasikia kuhusu mkatati huo, au hawakuweza kuelezea kwamba unahusu nini. Vivyo hivyo, wakati mkakati maarufu uliobuniwa na watanzania wenyewe wa kupunguza umasikini, ujulikanao kama MKUKUTA³ ukiwa unatekelezwa tangu 2005, wahojiwa 9 katika 10 walikuwa ama hawajawahi kuusikia au hawakuweza kuelezea unahusu nini. Hali hii inashangaza, hasa ukizingatia kwamba serikali na washirika wake wa maendeleo wamekuwa wakifanya jitihada kubwa kuutangaza mkakati huu kwa wananchi.

Vile vile idadi kubwa ya wahojiwa watu wazima katika Dar es Salaam hawazifahamu vizuri taasisi muhimu za kikanda ambazo Tanzania inajihusisha nazo. Kwa mfano,

³ Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini, kwa Kiingereza National Strategy for Growth and Reduction of Poverty

imebainika kuwa asilimia 72 ya wahojiwa ama kamwe hawajawahi kusikia kuhusu Jumua ya Afrika Mashariki (*East African Community*) au hawakuweza kueleza ni kitu gani japo jumua hiyo imekuwepo kwa zaidi ya muongo mmoja sasa tangu ulipofufuliwa.

Kielelezo cha 5: Uelewa wa wananchi kuhusu sera muhimu, taasisi




Chanzo cha data: Uwazi, Public Service Delivery Survey, Dar es Salaam, 2010

Jambo la 6: Wananchi walioelimika zaidi wanajua zaidi kuhusu sera

Uelewa kuhusu mambo mbalimbali yanayohusu sera unaonekana kuongezeka sambamba na kiwango cha elimu. Wahojiwa 9 kati ya 10 waliokuwa na kiwango cha elimu zaidi ya sekondari walishasikia kuhusu Kilimo Kwanza (asilimia 92) na waliweza kuelezea kuhusu mkakati huo, na kuhusu Jumua ya Afrika Mashariki wahojiwa asilimia 91. Uelewa kuhusu MKUKUTA ulikuwa wa chini kidogo hata katika kundi hili: ni sehemu tatu ya tano tu (asilimia 62) ya wahojiwa ndio waliweza kuelezea kuhusu mkakati huu.

Jinsi kiwango cha elimu cha mhojiwa kilivyokuwa chini ndivyo uelewa wake wa sera husika ulivyokuwa mdogo. Miongoni mwa wahojiwa ambao hawakuwa na elimu, hakuna hata mmoja kati yao aliyeweza kuelezea MKUKUTA ni nini, ni asilimia 5 tu waliweza kueleza kuhusu Kilimo Kwanza na asilimia 4 tu waliweza kueleza kuhusu Jumua ya Afrika Mashariki. Hata miongoni mwa wale wenye elimu ya sekondari, kama Kielelezo cha 6 kinavyonyesha, idadi kubwa kati yao hawakujua kuhusu sera hizi muhimu: asilimia 86 walisema kamwe hawajawahi kusikia kuhusu MKUKUTA, asilimia 73 walisema hawajawahi kusikia kuhusu Kilimo Kwanza, na asilimia 59 walisema hawajawahi kusikia kuhusu Jumua ya Afrika Mashariki.

Kielelezo cha 6: Uelewa wa wananchi wa sera za msingi, kwa kiwango cha elimu




Chanzo cha data: Uwazi, Public Service Delivery Survey, Dar es Salaam, 2010

Jambo la 7: Wananchi wanahudhuria mikutano zaidi kuliko kuchukua hatua wao wenyewe

Shinikizo kwa serikali au kwa mfumo wa utoaji huduma za kijamii kwa ajili ya kuleta mabadiliko na uwajibikaji zaidi lina nafasi nzuri zaidi ya kufanikiwa pale ambapo wananchi wanachagua kushiriki kikamilifu katika michakato muhimu. Viwango vya ushiriki katika njia zijulikanazo zaidi kwa uwezo wake wa kuleta mabadiliko vilikuwa mchanganyiko. Kama inavyoonekana katika Kielelezo cha 7, katika kipindi cha miezi 12 kabla ya utafiti huu kufanyika, wahojiwa wachache waliandika barua, au ujumbe mfupi wa simu au walipiga simu kwa mwendeshaji wa kipindi cha redio ili kutoa kero zao au malalamiko yao. Kwa upande mwingine, kiasi cha asilimia 37 ya wahojiwa walizungumza na afisa wa serikali kuhusu tatizo walilokuwa nalo na asilimia 59 walihudhuria mkutano wa kijamii katika eneo lao. Maswali ya utafiti hayakuchimba ndani zaidi kuhusu kiasi cha mafanikio kilichotokana na aina hizi za uchukuaji hatua, au kuchunguza iwapo wananchi wanatumia njia nyingine zaidi zisizo rasmi ili kuhakikisha mambo yanafanyika.

Kielelezo cha 7: Asilimia ya kaya zilizochukua hatua angalau mara moja katika kipindi cha miezi 12 kabla ya utafiti




Chanzo cha data: Uwazi, Public Service Delivery Survey, Dar es Salaam, 2010

Jambo la 8: Karibu nusu ya wahojiwa hawamjui Mbunge wao

Wabunge wanachaguliwa katika majimbo yao ya uchaguzi na wanatarajiwa kufanya kazi kwa manufaa ya wananchi waliowachagua na kuwajibika kwao. Ili jambo hili lifanikiwe watu wanapaswa kujua namna ya kufikisha malalamiko na mawazo yao kwa Mbunge wao. Hata hivyo, katika Dar es Salaam karibu nusu ya wahojiwa (asilimia 46) hawakujua jina la Mbunge wao, achilia mbali kupata fursa ya kukutana naye.

Katika utafiti huu, wahojiwa hawakuulizwa kwa nini hawakumfahamu Mbunge wao. Licha ya hali hiyo, asilimia 94 ya wahojiwa walikuwa na kitambulisho cha mpiga kura, ikionyesha kwamba walijiandikisha kupiga kura.

Kielelezo cha 8: Asilimia ya wahojiwa wanaomtambua Mbunge wao




Chanzo cha data: Uwazi, Public Service Delivery Survey, Dar es Salaam, 2010

Jambo la 9: Kuna maoni mchanganyiko kuhusu uwezekano wa kuadhibiwa kwa kuwa msemaji mno/kuonekana kimbelebele

Hofu ya kulipiziwa kisasi inaweza kupunguza nguvu ya wahojiwa kuchukua hatua katika kushughulikia matatizo ya upatikanaji wa huduma za jamii yanayowakabili au kushiriki katika kufanya maamuzi katika maeneo wanayoishi. Utafiti wetu (Kielelezo cha 9) umebaini kuwa zaidi kidogo tu ya nusu ya wahojiwa (asilimia 54) wanahisi kuwa hakuna uwezekano wa kuadhibiwa kwa kuzungumza yale yanayowakera, lakini sehemu mbili ya tano (asilimia 39) walionyeshwa kuwa na hisia kwamba kuna uwezekano mkubwa au kiasi fulani cha uwezekano wa kuadhibiwa.

Ukweli kwamba wahojiwa wachache ndio walisema walichukua hatua kutatua matatizo katika maeneo yao unaibua maswali iwapo njia na fursa zilizopo zinaeleweka vizuri kwa wananchi. Wahojiwa hawakuulizwa iwapo walijua mahali pa kupeleka malalamiko yao. Lakini, kwa kuwa wengi walisema hawamfahamu mwakilishi wao wa kisiasa na kwamba hawakujua vema kuhusu sera mbalimbali, uwezekano ni mkubwa kwamba njia za kuleta mabadiliko hazifahamiki kwa wananchi walio wengi. Kuna uwezekano pia kwamba wananchi wanazijua njia hizo ila wana mashaka kuwa kulalamika au kushiriki kwao hakutaleta mabadiliko yoyote.

Kielelezo cha 9: Maoni ya wahojiwa kuhusu uwezekano wa kuadhibiwa kwa kulalamikia huduma mbovu za kijamii au matumizi mabaya ya fedha za umma



Chanzo cha data: Uwazi, Public Service Delivery Survey, Dar es Salaam, 2010

Hitimisho


Muhtasari huu umeonyesha kwamba kwa kiasi kikubwa wananchi hawaridhishwi na namna serikali inavyoshughulikia mifumo ya utoaji huduma za msingi. Vile vile umeonyesha kwamba wananchi wana imani ndogo kwamba mamlaka zinafanya kazi kwa manufaa yao, kwamba watu wachache wanaelewa kuhusu sera muhimu nchini zinazohitaji ushiriki wao ili ziweze kufanikiwa, na kwamba miongoni mwa wale wasiozifahamu vizuri sera, wengi ni wananchi wasio na elimu/wenye elimu ya kiwango cha chini. Mwisho, ingawa kiwango cha tutoridhishwa na huduma za msingi za kijamii ni cha juu, watu wanaochukua hatua za kutoa taarifa, kushauriana na wengine, au kushiriki katika michakato inayoweza kusaidia kuhimiza mabadiliko katika maeneo yao ni wachache.

Serikali ipo ili kuwahudumia wananchi, na watu wana haki ya kudai uwazi na kuitaka serikali iwajibike. Hata hivyo, wananchi hawawezi kishiriki ipasavyo katika uongozi iwapo hawaelewi kinachoendelea katika maeneo yao au katika nchi, na kupata fursa za wazi za kurekebisha mambo. Japokuwa nyaraka za serikali zinatambua umuhimu wa uwazi, utekelezaji wake halisi unaonekana kulegalega. Huenda kubuniwa kwa mpango wa Ushirika wa Serikali Wazi (Open Government Partnership⁴), ambao unalenga kuifanya serikali kuwa wazi zaidi, bayana na shirikishi, na kujiunga kwa Serikali ya Tanzania na mpango huo hivi karibuni kutasaidia kuhimiza mabadiliko katika uhusiano wa dola na wananchi. Vinginevyo utahitajika msukumo mkubwa zaidi na udadisi wa wananchi unaoanzia ngazi za chini kwenda juu ili kubadili mfumo ulioshamiri kwa sasa wa mahusiano baina ya serikali na wananchi. Vyovyote vile itakuwa vema kuuliza maswali ya namna hii kila mwaka ili tuweze kufuatilia mabadiliko, au kukosekana kwa mabadiliko, kwa kipindi kirefu.

Kiambatisho: Sifa za wahojiwa katika utafiti

Mfumo uliotumika kuchagua sampuli ya wahojiwa kutoka manisipaa za Dar es Salaam ulikuwa wa madaraja na nasibu (*stratified random sampling*), ambapo wahojiwa waliochaguliwa walikuwa: Ilala (asilimia 32.7), Kinondoni (asilimia 33.7) na Temeke (asilimia 33.6). Wahojiwa walitembelewa na wakusanya data ambao waliuliza maswali kwa kutumia hojaji juu ya upatikanaji wa huduma za kijamii na masuala ya utawala. Sifa za msingi za wahojiwa zinaonyeshwa katika Kielelezo cha 10. Miongoni mwao kulikuwa na wahojiwa wanawake wengi zaidi kuliko wanaume. Karibu theluthi mbili ya wahojiwa walikuwa wanachama wa chama cha siasa. Zaidi kidogo tu ya nusu ya kaya za wahojiwa (asilimia 56) zilikuwa zimeunganishwa na gridi ya umeme ya taifa.

Kielelezo cha 10: Sifa za mhojiwa



Chanzo cha data: Uwazi, Public Service Delivery Survey, Dar es Salaam, 2010

4 Tazama www.opengovpartnership.org and www.opengovpartnership.go.tz